**MABORESHO OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI YAVUTIA MITAJI, AJIRA NA TEKNOLOJIA MIAKA MITATU YA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN**

Aprili 22, 2021, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, alilihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mara ya kwanza, pamoja na mambo mengine, aliwaeleza watanzania adhima yake ya kusimamia ukuzaji wa uchumi nchini.

Mhe. Dkt. Samia alisema kuwa ingawa uchumi ulikuwa unaendelea kukuwa na kuiweka nchi miongoni mwa kundi la nchi za uchumi wa kati, kulihitajika jitahada za makusudi za kukuza uchumi angalau kwa asilimia 8 kwa mwaka.

Miongoni mwa maamuzi makubwa aliyoyafanya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akilenga kuimarisha jitihatada za kukuza uchumi wa nchi ilikuwa ni kuanzisha Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji (OR-MU.

Hatua hiyo, iliyoambatana na kuziweka taasisi zinazoshughulika na uchumi wa nchi ambazo ni Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Tume ya Mipango, Ofisi ya Msajili wa Hazina (TR), Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA) na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kuongeza nguvu ya uratibu wa vyombo hivyo vinavyohusika na Mipango na Uwekezaji nchini.

Aidha, kuziweka taasisi hizo katika mwanvuli mmoja chini ya uangalizi wake kulilenga kumrahisishia Mhe. Rais Samia, kutoa maelekezo kwa urahisi na kuimarisha utendaji kazi wa taasisi hizo zinazotegemeana katika utekelezaji wa shughuli za Mipango na Uwekezaji.

Tangazo la Serikali namba 407 A na B (GN No. 407) la Juni 22, 2023 ndiyo lilirasimisha Hati ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji yenye jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mipango na Uwekezaji nchini.

Makala haya yanaangazia jitihada zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kukuza uchumi wa nchi tangu kuundwa kwa Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji inayoakisi mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita tangu kuingia madarakani.

**Uboreshaji wa Mazingira ya Uwekezaji na Biashara**

Kwa ujumla katika kipindi cha miaka mitatu tangu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan aingine madarakani, kumefanyika maboresho makubwa ya Kisera, Kisheria na Kikanuni yaliyochagiza kuimarisha mazingira ya Uwekezaji na Biashara.

Itakumbukwa kuwa, kulikuwa na malalamiko na viliyo kutoka kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuhusu mazingira ya bishara nchini, wakidai hayakuwa yenye kutabilika, yaliyogubikwa na mlolongo wenye taratibu nyingi katika kusajili vibali vya uwekezaji.

Malalamiko mengine yalihusu msululu wa sheria zisizosomana na utitili wa taasisi zinazoshughulikia uwekezaji zilizosajiliwa kwa sheria tofauti hali iliyosababisha kuzolota kwa shughuli za Uwekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Kwa kipindi cha miaka mitatu ya Serikali Rais, Dkt. Samia serikali imechukua hatua za makusudi za kuboresha mazingira ya Uwekezaji na Biashara ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Mosi, imepunguza au kuondoa zaidi ya ada/tozo 374 na kurekebisha zaidi ya sheria na kanuni 55 kutoka katika sekta za Uwekezaji; Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Maliasili, Utalii, Nishati, Madini, Viwanda na Biashara.

Kwa Mujibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji Mhe. Prof. Kitila Mkumbo (Mb.) hatua hiyo imeboresha mazingira ya Uwekezaji na kuvutia wawekezaji nchini na hali inayoiwezesha sekta binasfi kufanya kazi kwa ufanisi.

Aidha, Maboresho ya kisheria yameweka msisitizo katika mageuzi ya kitaasisi, ikiwemo kuunganisha baadhi ya mashirika ya Umma, kugawanya mashirika mengine, na kuyafuta yaliyoonekana kutokuwa na tija pamoja na kujenga mifumo kidigitali.

Maboresho mengine yaliyofanyika ni yanayohusu mifumo ya kielekroniki ikiwemo kuanzishwa kwa mfumo wa Dirisha Moja la Huduma *(Tanzania Electronic Investment Window -TeIW).*

*Mfumo huo* umewawezesha Wawekezaji kupata huduma za namba ya utambulisho wa utaifa, namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN), msamaha wa kodi, usajili wa kampuni, kibali cha kazi, hati ya ukaazi, haki ya umiliki na cheti cha uwekezaji.

Mathalani, matumizi ya mfumo yamepunguza muda (siku) za kupata huduma, Cheti cha Usajili wa Sehemu za kazi kutoka siku 14 hadi siku 1, hatua hiyo imesaidia wawekezaji kuokoa muda na gharama za kusajili kapuni *(Registration Certificate*.

Vile vile matumizi ya *TeIW yamepunguza* muda wa kutoa Leseni kutoka siku 28 hadi siku 3 ikiwa Mwekezaji atakidhi matakwa ya Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (Compliance License), na muda wa maombi ya Vibali vya Kazi umepungua kutoka siku zaidi 14 za kisheria kufikia wastani wa siku 3 hadi 7 ikiwa mwekezaji atakidhi vigezo vyote.

Wakati huo huo, Serikali imeanzisha Idara inayohusika na Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 ili kuchochea kasi ya uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara, kuhudumia sekta binafsi na kutatua changamoto zilizobainishwa katika Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Biashara (MKUMBI).

Serikali Ofisi ya Msajili wa Hazina (TR), yamefanyika maboresho ya kimuondo na kiutawala katika kipindi hicho cha miaka mitatu ya serikali ya awamu ya Sita ambayo yamechangia ufanisi wa kiutendaji na ongezeko la mapato ya nchi.

Mapato yaliyoongezeka yametokana na kukusanya mapato yasiyo ya kodi yanayojumuisha Gawio (dividends), Michango ya 15% ya Mapato ghafi na mapato mengineyo.

Katika kipindi cha Miaka mitatu ya Mhe. Dkt. Samia mapato yasiyo ya kikodi (Non-Tax Revenue) yameongezeka kutoka shilingi billioni **637.66** mwaka 2021 hadi shilingi Trilioni **1.00839** mwaka 2023 ambalo ni ongezeko la asilimia 58.14.

Kama hiyo haitoshi, katika kipindi kinachoishia Februari 2024, Serikali imefanikiwa kuongeza umiliki wa hisa katika Kampuni ya Madini ya Almasi ya Williamson kutoka asilimia 25 hadi asilimia 37.

Mafanikio hayo ni uthibitisho wa adhma ya Serikali ya Awamu ya Sita, yaliyolenga kuyataka mashirika ya Umma kujiendesha kwa ufanisi na faida.

Sambamba na hilo, serikali imesaini mikataba ya ubia iliyoiwezesha nchi kumiliki kwa kuwanzia kiwango cha asilimia 16 ya hisa zisizohamishika kwa kampuni saba.

Kampuni za Faru Graphite Corporation; Kudu Graphite Corporation, Dumagraphite Company Limited, Mamba mineral Corporation Limited, Sota Mining Corporation, Nyati Minerals Limited pamoja na Tembo Nickel Refining Limited.

Eneo lingine ni la uimarishwaji wa mashirika ya Umma ambapo zaidi ya shillingi Trillioni 5.5 zimeongezawa kama mtaji ili kuyawezesha Mashirika ya TANESCO, TPDC, TCB na TADB kujiendesha kibiashara hatimaye kupata faida na kuchangia kwenye pato la Taifa.

Katika miaka hii mitatu ya Serikali ya Rais Dkt. Samia imeweka wazi kuwa TANESCO iliongezewa shillingi trillioni 2.419, ili kuwezesha ufanisi wa shirika hilo kwa kuboresha njia za usafirishaji wa umeme na miundombinu ya uzalishaji, shirika la TPDC liliongezewa shillingi trillioni 2.752 kuboresha tafiti za mafuta na gesi ili kufanikisha uchimbaji wa mafuta na gesi, TADB shillingi bilioni 208 kukopesha wawekezaji waliyo katika kilimo, na Benki ya TCB shillingi billioni 131.

Aidha, ndani ya miaka mitatu ya Mshemiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan serikali imeleta miradi yenye thamani ya dola za Marekani milioni 1171.97 kupitia EPZA na imeongeza ukuaji wa mauzo ya nje kwa thamani ya dola za Marekani Milioni 397.64 na kuzalisha ajira 20,674 iliyopatikana na baada ya Miradi 45 kusajiliwa katika maeneo mbalimbali nchini kupitia leseni za EPZ na SEZ.

Aidha, Miradi iliyosajiliwa imeleta mitaji katika sekta za uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na Kilimo *(Agro Processing)*, Viwandani *(Industrial Activity),* Bidhaa za Mifugo, Bidhaa za Kemikali, Bidhaa za Madini na Bidhaa za Mazao ya Misitu.

Vile vile Serikali imetenga hekari 4039 katika Mkoa wa Manyara Dodoma, Pwani na Ruvuma kwa ajili ya uwekezaji.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita, kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kutoa takwimu rasmi na pia kutekeleza miradi mipya ya kuimarisha takwimu kwa maendeleo ya nchi.

Aidha, takwimu zilizofanywa na NBS zimesaidia kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa sera, mipango na programu mbalimbali za maendeleo za kitaifa na kimataifa zikiweme Dira ya Maendeleo ya Afrika 2063, Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki 2050 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030.

Baadhi ya tafiti zilizofanyika katika kipindi cha miaka mitatu ni pamoja na; Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022, Utafiti wa Viashiria na Matokeo ya UKIMWI Tanzania wa Mwaka 2022/23, Utafiti wa Athari za Upatikanaji wa Nishati Endelevu wa Mwaka 2021/22.

Tafiti nyingine ni, Utafiti wa Huduma za Kifedha wa Mwaka 2023, Utafiti wa Shughuli za Kiuchumi na Kijamii wa Mwaka 2023/24 Tanzania Bara, Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2022/23, Utafiti wa Kutathmini Upatikanaji wa Huduma za Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2023, na Utafiti unaoendelea wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanyakazi wa Mwaka 2024.

Tafiti hizo zimeonesha kuwepo kwa onegezeko la idadi ya watalii walioingia nchini kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 1,805,367 mwaka 2023 hasa baada ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kutangaza utalii wa nchi yetu ndani na nje kwa kushiriki katika filamu ya Royal tour.

Mafanikio mengine yanatokana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 ambapo Serikali ya imeendelea kutoa elimu juu ya faida zitokanazo na matokeo ya Sensa ya kama ilivyokusudiwa kwa kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Matumizi ya Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Katika kuhakikisha nchi inakuwa na Maendeleo endelevu, Serikali ya awamu ya sita imefanikiwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na kuainisha maendeleo yaliyopatikana kupitia utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ambao umefanikiwa kwa asilimia 60 hadi kufikia mwaka 2022 hasa katika sekta za huduma za jamii.

Mathalani, tathimini hiyo inaonesha kywa kuna ongezeko la wanafunzi wanaoandikishwa, kutoka asilimia 69 mwaka 1999 hadi asilimia 97 mwaka 2022, baada ya serikali kuongeza shule nyingi za msingi na sekondali hatua inayomwezesha kila mtoto kuwa na uhakika wa kusoma.

Vile vile, kuna ongezeko la upatikanaji wa huduma za Afya,  uliyoongezeka kwa asilimia 21.6 mwaka 2022, na kupungua kwa idadi ya watoto wanaosumbuliwa na utapiamlo na uzito pungufu kutoka asilimia 48.3 na 25.3 mwaka 1999 hadi wastani wa asilimia 30 na 12 mwaka 2022.

Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita imefanikiwa kuanza kwa zoezi la maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 pamoja na Mpango Elekezi wa Muda Mrefu.